Mchambuzi: Evarist Chahali

Imechapishwa: Mei 19, 2020

Glasgow, Uskochi.

Utangulizi:

Kama unafuatilia mabandiko yangu kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter, katika siku za hivi karibuni nimekuwa nikiongelea sana mustakabali wa Rais John Magufuli kuhusiana na jinsi anavyoshughulikia janga la korona huko Tanzania.

Katika makala hii ambayo imeandaliwa kama taarifa ya kiusalama (intelligence report), uchambuzi wa kiintelijensia unafanywa kwa kutumia mbinu 4. Lengo la kutumia mbinu nyingi kiasi hicho ni kutanua wigo wa uchambuzi.

Mbinu hizo ni kama zifuatavyo

1. ***Tafakuri Jadidu na Ujenzi wa Dhanio (Creative Thinking and Hypothesis Generation)***: Kwa kifupi, katika mbinu hii ninakagua hisia husika na kujenga dhanio. Kwahiyo hapa kuna hatua mbili. Ya kwanza ni ***Kukagua Hisia Husika*** (***Key Assumptions Check*** - ***KAC***) ambayo kimsingi ni kutambulisha dhana husika, ambayo katika somo hili ni ***mustakabali wa urais wa Magufuli kuhusiana na janga la korona***. Kwa kuangalia tu mustakabali wa urais wake inamaanisha kuwa "kuna namna." Ni kama kuongelea wosia ilhali mtu yupo hai. Yawezekana ni maandalizi tu **endapo** mhusika "ataondoka," kitu ambacho katika mila za Kiafrika ni kama uchuro, au ni maandalizi kwa vile **kuna dalil**i za mtu kuondoka, kwa mfano yu mgonjwa mahututi. Hatua ya pili ni "***Hypothesis Generation***." Hapa ninajenga dhanio, ambao katika somo hili ni kwamba "***KORONA ITAMUONDOA MAGUFULI MADARAKANI.***"
2. ***Kutengeneza Maana Katika Taarifa Ngumu (Making Sense of Complex Data)***: Kwa vile Magufuli amekuwa madarakani kwa miaka mitano sasa, na wanasema "kwenye siasa, wiki tu ni sawa na umri wa mtu mzima," ni dhahiri kuwa kuna mengi mno ya kuyaangalia kuhusu urais wa Magufuli, hususan alikotoka, alipo na aendako. Lakini kwa minajili ya kuokoa muda na nafasi, katika mbinu hii nitaangalia maeneo mawili tu. La kwanza ni ***Tathmini ya Mienendo (Pattern Analysis)***, na la pili ni ***Kulinganisha Matukio Yanayohusiana (Comparative Case Analysis)***

3. ***Kupima Dhanio (Hypothesis Testing):*** Hapa kuna mbinu moja tu, nayo ni ***Tathmini ya Madhanio Yanayoshindana (Analysis of Competing Hypotheses).***
4. ***Ujenzi wa Mazingira (ya kufikirika) Na Kuyafanyia Tathmini (Generating and Evaluating Scenarios):*** Kwenye kutengeneza mazingira (ya kufikirika) nitatumia mbinu mbili. Ya kwanza ni ***Mchakato wa Roboduara (Quadrant Crunching)*** na ya pili ni ***Kujivika Upinzani/Uadui (Red Teaming).***

Baada ya utangulizi huo ambao umejikita zaidi kwenye kutanabaisha mbinu mbalimbali za uchambuzi wa kiintelijensia nitakazozitumia kwenye uchambuzi huu, sasa nieleze kwa kifupi kwanini nimeshawishika kuandika uchambuzi huu na pengine kwanini uchambuzi huu una umuhimu (labda si kwako bali kwangu au kwa kila anayeguswa na mustakabali wa Tanzania yetu).

Kwa upande mmoja, dunia inapitia katika moja ya vipindi vigumu kabisa kuwahi kushuhudiwa na kizazi hiki. Tumekuwa tukisikia kuhusu majanga yaliyowahi kutokea huko nyuma kama Spanish Flu au Black Death lakini katika kizazi chetu hatujawahi kushuhudia kitu kinachokaribiana na janga la korona.

Kwa bahati mbaya, hakuna uhakika endapo korona itadhibitiwa na kuondoka. Unapoona mataifa tajiri na makubwa kama Marekani na hapa Uingereza “yanapelekeshwa” na janga hili bila kuwepo ufumbuzi, basi ni rahisi tu kuelewa kuwa hali ni ngumu zaidi kwa nchi masikini kama Tanzania yenye changamoto lukuki.

Kwa vile hakuna chanjo wala tiba ya korona, tegemeo kubwa kwa sasa ni hatua thabiti za kupunguza maambukizi. Lakini ili hatua hizo ziwezekane ni lazima kuwepo uongozi thabiti. Korona ni janga la kisayansi lakini pia linalohitaji ufumbuzi kwa njia za kisiasa. Hapana, sio kuingiza siasa kwenye sayansi bali kutumia siasa kusisaidia sayansi kukabiliana na janga hili.

Mafanikio yaliyofikiwa katika baadhi ya nchi zinazofanya vema kupambana na korona – kwa mfano Ujerumani, New Zealand na Korea ya Kusini, na kwa Afrika, nchi kama Rwanda, Uganda, Kenya, Afrika Kusini, Senegal, Nigeria na Ethiopia –

yamechangiwa zaidi na “siasa kuisapoti sayansi” badala ya kuwa kikwazo.

Kwa Tanzania, hali ni tofauti. Tangu awali, yaani kabla serikali haijatamka rasmi kuhusu janga hilo kuingia nchini humo, kulikuwa na ishara kuwa sio tu siasa ingekuwa mbele ya sayansi bali pia siasa ingekwaza sayansi.

Siku moja baada ya “korona kuingia Tanzania,” nilifanya uchambuzi HUU ambao pamoja na mambo mengine ulionyesha hofu yangu kuhusu mwenendo wa serikali kushughulikia janga hilo.

Ikumbukwe kuwa Machi 16 mwaka huu, siku hiyohiyo ambayo Waziri wa Afya Ummy Mwalimu alitangaza “kuingia kwa korona nchini Tanzania,” Rais Magufuli alihutubia akijigamba kuwa korona haijaingia nchini humo na kuwatoa hofu wananchi bila kueleza hatua za msingi za serikali yake kukabiliana na janga hilo.

Lakini pia siku hiyo hiyo ilishuhudia msemaji mkuu wa serikali, Dkt Abbas akiwadhihaki wananchi walioonekana kuwa na hofu kuhusu ugonjwa huo hatari.

Lakini uthibitisho kuwa siasa sio tu ingekuwa mbele ya sayansi katika kushughulikia janga hilo bali pia siasa ingekuwa kikwazo, mara baada ya tangazo la Waziri Ummy, kauli za Rais Magufuli zimekuwa na madhara makubwa pengine zaidi ya virusi vya korona.

Kwa kuokoa nafasi na muda, misimamo mitatu ya Rais Magufuli imekuwa kama ifuatavyo.

1. **Tusitishane**: korona sio “ishu kubwa kihivyo” kwa sababu hata “ukimwi na malaria huua watu kama ilivyo kwa ajali.” Kwahiyo hapa Rais Magufuli anataka Watanzania waichukulie korona kama ugonjwa wa kawaida tu.
2. **Korona ni kazi ya shetani**: Na njia ya kupambana na kazi ya shetani ni kumtegemea Mungu. Kwa sie waumini, Mungu ni wa kumtegemea kwenye kila jambo lakini si kwa kuzembea kutumiza wajibu kisha kumtegemea Mungu. Mungu huwasaidia wanaojisaidia. Mungu ametujali uwezo wa kufahamu sayansi inayotuwezesha kukabiliana na magonjwa. Kwa Rais Magufuli, korona sio suala la kisayansi

bali la kiroho. Kwa mtazamo wake, vita dhidi ya korona ipiganwe makanisani na misikitini badala ya kwenye maabara.

3. **Mvuke unaua virusi vya korona**: Rais Magufuli ni mwanasayansi, au angalau hivyo ndivyo tunavyoaminishwa. Lakini kwa kuangalia matukio mawili yanayohusu sayansi – "tiba ya kikombe cha Babu Ambi" na hiyo "tiba ya mvuke" inaweza kumfanya mtu ahoji kama hiyo Shahada ya Uzamifu ya Rais Magufuli sio feki.
4. **Korona ni mkakati wa mabeberu**: Moja ya vitu ambavyo Rais Magufuli amefanikiwa sana ni kurejesha "chuki dhidi ya nchi za Magharibi," kwa maana ya kurejea kwa neno "mabeberu." Lakini takriban kila mara, nenu "mabeberu" hutumika kama kisingizio au utetezi dhidi ya lawama au malalamiko halali. Serikali ya Rais Magufuli inapokosolewa kuhusu rekodi yake kwenye haki za binadamu, kwa mfano, hukimbilia kulaumu "mabeberu." Na katika suala la korona, hivi karibuni zaidi wa Rais Magufuli ni kuwalaumu "mabeberu" kwa madai kuwa wametoa vipimo vya kupimia korona vyenye walakini.

Baada ya kuangalia mitazamo hiyo ya Rais Magufuli, sasa nigusie kwanini suala la korona lina upekee wa aina yake kwa Rais Magufuli. Bila kuingia kwa undani, kwa miaka mitano sasa, Rais Magufuli amekuwa mtu wa kuona kila takwa lake linatimia. Ilianzia kwenye kuzuwia shughuli halali za vyama vya siasa. Ikahamia kwenye kuviziba midomo vyombo vya habari. Ikaja kwenye kuzuwia matangazo ya moja kwa moja ya bunge. Ikaja kwenye kuwadhibiti wakosoaji wake – Ben Saanane "akapotea" kabla ya Tundu Lissu kunusurika kuuawa. Sambamba na hayo akaanzisha soko la kununua wapinzani. Na baada ya kuwanunua akawarejeshea ubunge na wengine akawapa zawadi za vyeo serikalini.

Kwa kifupi, kiongozi huyu ambaye wakati flani alieleza bayana lengo lake la kuja kuwa kiongozi mkuu wa malaika, alishaanza kupata hisia kuwa yeye ni mungu-mtu flani. Ukichanganya na jinsi "wapambe" walivyokuwa wanammwagia sifa na kumtukuza, akajenga imani kwamba kila atakalo huwa.

Kwahiyo ni rahisi kuelewa kwanini janga hili la korona linampa shida sana. Hajawahi hata mara moja kukumbana na “adui aliyemzidi uwezo.” Kwake, kila adui aliweza kudhibitiwa na hata kuangamizwa ilipobidi.

Lakini pia kuna upande mwingine wa suala hili. Kwa vile Rais Magufuli amejijengea taswira hiyo ya kutoshindwa katika kila jambo, na “wapambe” wake wakijibidiisha kuwaaminisha Watanzania hivyo, endapo korona itamshinda inaweza kupelekea kile Waingereza wanaita “kufungua kopo la minyoo (*opening a can of worms*)”

Ili kuelewa hili vizuri ni muhimu kurejea jitihada kubwa zilizofanywa na Rais Magufuli kujenga na kuimarisha siasa za chuki, siasa zilizopelekea wapinzani wake ndani na nje ya chama hicho kutendewa vibaya. Rejea yaliyowakuta akina Mzee Makamba na mwanae January, Kinana, Nape na wengineo, ilhali mhanga mkubwa zaidi wa siasa za chuki za Rais Magufuli akiwa Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Bernard Membe, ambaye Rais Magufuli ameamua afukuzwe uanachama wa CCM. Kosa pekee la kada huyo mkongwe wa chama hicho tawala ni tetesi kuwa anataka kuwania urais kwa tiketi ya chama hicho, ikimaanisha angekuwa mpinzani wa Rais Maguguli.

Sasa nihamie kwenye mbinu mbalimbali za kuchambua mustakabali wa Rais Magufuli. Mbinu hizo ni kama zifuatavyo

1. Tafakuri Jadidu na Ujenzi wa Dhanio (Creative Thinking and Hypothesis Generation): Hapa kuna hatua mbili. Ya kwanza ni Kukagua Hisia Husika (Key Assumptions Check - KAC). Hatua ya pili ni “Hypothesis Generation.”

Hisia zetu huathiri mitazamo yetu na jinsi tunavyochanganua mambo mbalimbali. Mara nyingi hisia hizi huwa nje ya uwezo wetu. Lakini kwenye ushushushu, hisia hizi huchangiwa na uwezo binafsi wa shushushu husika. Hisia hizi zina nafasi muhimu katika kufanya chambuzi za kiintelijensia.

Kufahamu hisia kuhusu suala husika, ni muhimu kuzitambua na kuzikagua. Kwahiyo, hapa nitaeleza hisia zangu kuhusu Rais Magufuli.

Hisia ya kwanza ni kwamba Rais Magufuli analichukulia janga la korona kama adui yake binafsi. Na siku zote amefanikiwa kuwashinda maadui zake, angalau kwa ndani ya Tanzania. Kwahiyo kichwani ana picha ya ushindi dhidi ya adui hiyo.

Hisia ya pili ni kwamba kwa vile janga la korona linakaribia mwezi wa tatu sasa tangu liingie Tanzania, kwa mara ya kwanza, Rais Magufuli anakabiliana na “adui mbishi” ambaye sio tu haonyeshi dalili ya kumuogopa “Jiwe” bali pia hana dalili ya kuondoka leo au kesho.

Hisia ya tatu ni kwamba Rais Magufuli ana hasira dhidi ya janga la korona, si kwa vile linaangamiza watu na huenda likaangamiza watu wengi zaidi, bali ana hasira kwa sababu anaona janga hili linakwamisha “ndoto zake kuhusu Tanzania aitakayo.”

Hisia ya nne ni kwamba Rais Magufuli kutochukuliwa janga la korona kwa uzito mkubwa ni kutokana na chuki zake. Kuna ushahidi mwingi kuwa Rais Magufuli amekuwa muumini wa siasa za chuki. Na kuthibitisha kuwa ana chuki, tangu mgonjwa wa kwanza afariki kwa korona, Rais Magufuli hajawahi kutoa pole kwa wafiwa. Pole pekee alizotoa ni kwa viongozi waliofariki bila umma kuambiwa kuwa wamefariki kwa korona.

Hisia nyingine ni kwamba kadri idadi ya vifo itakavyozidi kuongezeka ndivyo kadri sapoti ambayo bado anayo ndani ya CCM itazidi kupungua.

Ni rahisi kwa “wapambe” wake kushikama nae muda huu kwa sababu janga hilo halijawaathiri, lakini yayumkinika kuamini kuwa pindi nao wakianza kupoteza ndugu, jamaa au marafiki kutokana na janga hilo, watabaini kuwa Rais Magufuli “si rafiki mwema bali adui aliyesababisha vifo hivyo.”

Hisia ya sita ni kwamba maadui wa Rais Magufuli ndani ya CCM na wa nje ya CCM wataungana dhidi yake kadri idadi ya vifo vya korona itakavyozidi kuongezeka.

Hisia ya saba ni kwamba Tanzania itazidi kutengwa na majirani zake huku Jumuiya ya kimataifa nayo ikizidisha shinikizo. Shinikizo la ndani na hilo la nje litamfanya Rais Magufuli kuchukua maamuzi ya kukurupuka ni kiongozi anayeendeshwa

na jazba) ambayo yatauweka urais wake katika wakati mgumu zaidi.

Hisia nyingine ni kwamba kwa vile Rais Magufuli hajawahi kushindwa, angalau kwenye mapambano yake ya ndani ya nchi, hakuna dalili kwa yeye kusalimu amri kwa janga la korona, kwa maana kwamba haitarajiwi akatokea kubadili msimamo. Hata hivyo, vifo vya watu wa karibu yake vitamfanya akose mwelekezo, na kufanya maamuzi "erratic" yatakayowaongezea nguvu wapinzani wake ndani na nje ya CCM kushinikiza ang'olewe.

Hisia nyingine ni kwamba kadri watakavyojitokeza watu wa "kumkimbia" (yaani "wapambe" watakaomhasi) ndivyo kadri Watanzania watakavyokuja kufahamu ni kwa jinsi gani janga la korona limeiathiri nchi yao, sambamba na kupata ushahidi kwa jinsi gani Rais Magufuli ni mtu katili asiye na chembe ya huruma kwa Watanzania.

Na hisia hizo zinawezesha kutengeneza dhanio kuwa JANGA LA KORONA LITAMUONDOA RAIS MAGUFULI MADARAKANI

2. Kutengeneza Maana Katika Taarifa Ngumu (Making Sense of Complex Data):

Takriban kila kitu kinachopelekea shushushu afikie hatua ya kukifanyia uchambuzi, huwa kimepitia hatua moja au zaidi. Na hatua hizo hueleza mahusiano kati ya mtu/watu husika, eneo/maeneo husika, shughuli, nk. Kuna njia kadhaa za kumwezesha shushushu kuwasilisha taarifa husika. Njia hizo ni kama ifuatavyo:

Tathmini ya Mienendo (Pattern analysis)

Njia hii huwezesha kufuatilia mienendo inayojichomoza na iliyopo, matukio yanayohusiana na mienendo hiyo, maeneo husika, tabia za mhusika/wahusika, nk.

Kusoma mienendo humwezesha shushushu kubashiri "kinachoendelea" na kinachotarajia/yanayotarajiwa kutokea.

Kutengeneza mlolongo wa matukio humwezesha shushushu kujenga picha kubwa zaidi ya kinachoendelea/yanayoendelea na nani anahusiana na nani katika wakati husika.

Katika kuangalia mustakabali wa Rais Magufuli kuhusiana na janga la korona, orodha ya matukio ni ndefu mno kuijumuisha hapa, lakini jinsi alivyoshughulikia majanga yaliyoikumba Tanzania huko nyuma inaweza kueleza “kinachoendelea” muda huu.

Nukuu hii chini ni kutoka kwenye blogu yangu ya Kulikoni Ughaibuni

Kuna mfululizo wa matukio yanayoashiria bayana kuwa Rais Magufuli ana mapungufu ya kiuongozi kila wakati Tanzania yetu inapokumbwa na majanga. Tukio kubwa zaidi ni lile la tetemeko la ardhi Kagera ambapo kwanza alipuuza kutembelea wahanga kwa siku kadhaa, na alipoamua kuwatembelea, akaishia "kuwasemea ovyo" kwa kudai si yeye aliyesababisha tetemeko hilo.

Kwanini tukio hili ni kubwa zaidi? Si tu kwa vile liliathiri watu wengi lakini pia kwa sababu Magufuli anatokea eneo hilo. Kwa lugha nyingine, kama anaweza "kuwafanyia hivyo ndugu zake," kwaninia shindwe kwa "watu baki"?

Matukio mengine ambayo yalipuuzwa na Magufuli ni pamoja na maombolezo ya askari wetu waliouawa huko DRC walikokuwa wakishiriki operesheni za kikosi cha Umoja wa Mataifa cha kulinda amani nchini humo. Licha ya kuwa Amiri Jeshi Mkuu, hakushiriki kuaga miili ya mashujaa wetu hao.

Janga jingine kwa taifa ambalo Magufuli alilipuuza nivifo vya wanafunzi kadhaa wa shule ya St Lucky huko Arusha

SAMIA AONGOZA WAOMBOLEZAJI KUAGA MIILI YA WANAFUNZI ARUSHA

5:34:00 PM / Unknown / NEWS / No comments /

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan leo tarehe 8-May-2017 ameongoza mamia ya wananchi wa mkoa wa Arusha na Mikoa ya Jirani katika kuaga miili ya wanafunzi 32,walimu Wawili na pamoja na Dereva Mmoja wa shule ya Lucky Visent katika uwanja wa Shekh Amri Abeid Jijini Arusha waliopata ajali katika eneo la Rhotia wilayani Karatu mkoani Arusha.

Kadhalika, Magufuli alipuuzia janga jingine lililotokea kanda ya Ziwa ambapo mamia walifariki katika ajali ya kivuko cha MV Nyerere

MAJALIWA ASHIRIKI MAZISHI YA WALIOFARIKI DUNIA KATIKA AJALI YA KIVUKO CHA MV NYERERE

HABARI PMO 9/23/2018 05:57:00 PM

Na akapuuzia pia janga la mlipuko wa lori la mafuta uliopolekea vifo kadhaa

Na kama alivyopuuzia janga la vifo vya mashujaa wetu waliouwa huko DRC, Magufuli hakutokea kwenye kuaga miili ya polisi waliouawa huko MKIRU, licha ya kuwa Amiri Jeshi Mkuu

Katika janga hili la korona, mwenendo wake tangu mwanzo umekuwa ni mwendelezo wa dharau zake kwa majanga yanapolikumba taifa letu. Baada ya Waziri wa Afya Ummy Mwalimu kutangaza kuwa korona imeingia Tanzania,

ilimchukua Magufuli siku 10 hivi kuongea lolote kuhusu janga hilo.

Na alipofungua mdomo wake, akaongea vitu vya ovyo kabisa. Akiwa Kanisani, aliweka kando uanasayansi wake na kudai kuwa "ukimwi unaua, malaria inaua, na ajali pia zinaua," na kusema kuwa "tunatishana sana (kuhusu korona). Haya si maneno ya kuyatarajia kutoka kwa kiongozi mkuu wa nchi ambaye pia ni mfariji mkuu.

Evarist Chahali

✓@Chahali

"Ukimwi unaua. Malaria inaua. Ajali zinaua... Tusitishane... Nendeni mkalime..."
~ @MagufuliJP, Machi 22, 2020

7

2:33 PM - Mar 23, 2020

Baadaye akahutubia taifa na kuendelea kutoa ujumbe usio na tija.

Jifunze Kiswahili@JifunzeSwahili

RAIS MAGUFULI: TUSITISHANE KUHUSU #COVID19 TUCHAPE KAZI

> Amesema tusitishane kwani hakuna ripoti ya kifo cha #Covid19 nchini

> Amesema hatuwezi kusalimu amri kwa ugonjwa huu wa #Covid19 na tukashindwa kuendeleza uchumi wetu

Zaidi, soma https://jamii.app/MagufuliCorona

Rais Magufuli: Watu tusitishane, Mpaka sasa Corona haijaua mtu...

"#Corona mpaka sasa hivi haijaua mtu hata mmoja hapa #Tanzania...lakini tunatishana sana...ninaanza kupata wasiwasi kwamba inafika mahali mpaka watu tumeanza kumsahau Mungu," - Rais Magufuli...

jamiiforums.com

10:59 AM - Mar 22, 2020

Baada ya ukimya wa siku kadhaa akaibukia tena huko Dodoma ambapo wakati taifa likiwa kwenye hofu na mashaka ya janga hilo la korona, mkuu huyo wa nchi akaonekana akifanya mzaha kwa kujilaza kwenye mawe.

Na majuzi alionekana akipuuza ushauri wa kitaalamu dhidi ya maambukizi ya korona unaowataka watu kuepuka mikusanyiko.

Na hii ilikuwa baada ya matukio makubwa mawili huko Dodoma yaliyosababisha mkusanyiko - kikao cha baraza la mawaziri na wakuu wa vyombo vya dola, na baadaye kupokea ripoti za TAKUKURU na CAG.

Kwa minajili ya kumbukumbu, mwaka juzi, mwanasiasa

nguli wa upinzani Tundu Lissu alihoji kasumba hiyo ya Magufuli kujitenga na majanga ya kitaifa.

Tathmini ya Matukio Yanayohusiana (Comparative Case Analysis)

Mmoja wa madikteta wanaofananishwa sana na Rais Magufuli ni Mobutu Sese Seko wa iliyokuwa Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Congo). Kinachowafanya watu wengi kumfananisha Rais Magufuli na Mobutu ni kasumba inayozidi kujengeka ya "kilimbikiza kila kitu huko Chato."

Moja ya kumbukumbu muhimu za utawala wa kidikteta wa Mobutu ulikuwa kukigeuza kijiji alichozaliwa cha Gbadolite kuwa kama jiji lenye kila kitu cha kukidhi matakwa yake. Na katika miaka mitano ya utawala Magufuli, Chato imegeuka kuwa kila kitu, kuanzia kuwa na mbuga ya wanyama jirani hadi kujengewa uwanja wa ndege wa kimataifa.

Kingine kinachomfananisha Rais Magufuli na Mobutu ni sabau walizotumia kudhibiti wapinzani wao mwanzoni mwa uongozi wao. Mara baada ya mapinduzi yaliyomwingiza madarakani mwaka 1965, Mobutu alipiga marufuku shughuli za kisiasa akiwatuhumu wanasiasa kwa kuiangusha nchi hiyo. Kadhalika alishinikiza nguvu za bunge ziwe muhuri tu. Vilevile, dikteta huyo aliangamiza wapinzani wake na yeye akawa ndio kila kitu.

Kama ilivyokuwa kwa Mobutu, Rais Magufuli "aliharamisha" shughuli za vyama vya upinzani akidai kuwa "sasa ni wakati wa kuchapa kazi na sio kufanya mikutano au maandamano ya kisiasa." Lakini kama ilivyokuwa kwa Mobutu, shughuli za kisiasa kwa chama tawala CCM sio tu zimeendelea bila bughudha kutoka kwa vyombo vya dola bali pia zimekuwa zikipewa ulinzi wa kutosha. Utawala wa Rais Magufuli utakumbukwa na vyama vya upinzani kama uliowafanya viongozi na wanachama wa vyama hivyo kutumia muda mwingi wakiwa jela kama sio mahakamani kwa kesi zisizo na msingi. Kadhalika, kama ilivyokuwa kwa Mobutu, miaka mitano ya utawala wa Rais Magufuli imeshuhudia mauaji kadhaa ya viongozi na wanachama wa upinzani.

Kadhalika, kama Mabuto alivyofanya jitihada kubwa za kujitengenezea mazingira ya kuwa rais wa milele, Rais Magufuli pia amekuwa akifanya jitihada kubwa kujitengenezea mazingira yanayoweza kumrahisishia kinachoaminika kuwa dhama yake ya kutawala milele. Kwa upande mmoja amefanikiwa kukifumua chama tawala CCM na kupandikiza watu wake, huku jumuiya mbili muhimu za chama hicho, ya Vijana (UVCCM) na ya Wanawake (UWT) zikiwa chini ya uongozi wa watu wa karibu naye. Mwenyekiti wa UVCCM Taifa ni mpwa wake.

Kingine kinachomfananisha Rais Magufuli na Mobutu ni kubadili mawaziri mara kwa mara. Na kama ilivyokuwa kwa Mobutu ambapo mabadiliko hayo ya mara kwa mara yalihusiana na zaidi na kuimarisha nafasi ya uongozi wake kwa kuwaondoa mawaziri aliodhani ni tishio kwake, ndivyo ilivyokuwa kwa Rais Magufuli ambapo wanasiasa vijana wenye mvuto mkubwa wa kiasiasa kama vile January Makamba na Nape Nnauye waliondolewa madarakani kionevu.

Kingine kinachomfananisha Rais Magufuli na Mobutu ni tabia ya dikteta huyo wa Zaire kupenda kunyanyaswa watendaji wake, kuwaadhibu na hatimaye kuwapa vyeo baadhi yao. Ni mbinu yenye ufanisi kwenye kumfanya mtendaji kuwa “mateka wa kisiasa” kwani anapoondolewa madarakani anaamini kuwa ndio mwisho wake, lakini ghafla “anarushiwa kamba ya kumwokoa kisimani.” Rais Magufuli pia ametokea kuwa mahiri wa kuwaondoa madarakani watendaji wake kadhaa kabla ya kuwapa promosheni tena, hali inayowafanya watendaji hao kuwa “mateka wake wa kisiasa.”

Mifano muhimu zaidi ni ya Waziri wa Sheria na Katiba, Mwigulu Nchemba ambaye awali aling’olewa Uwaziri wa Mambo ya Ndani akituhumiwa kuwa na makosa 13 ikiwa ni pamoja na ufisadi. Hata hivyo, Mwigulukwa kufahamu udhaifu wa Rais Magufuli wa kupenda kusifiwa, aligeuka kuwa msifiaji maarufu zaidi wa Rais Magufuli ambapo ilikuwa nadra kupita wiki bila mwanasiasa huyo kudakia hoja mitandaoni kwa ajili ya kumsifia Rais Magufuli. Na fursa muhimu iliwadia kwake kwa namna mbili.

Kwanza ni pale Rais Magufuli alipokuwa anashutumiwa na watu wengi kwa uamuzi wake wa “kujificha” huko Chato huku taifa

likiwa kwenye mapambano dhidi ya janga la korona. Mwigulu, katika namna ya kipekee, alifanya utetezi mkubwa bungeni akidai “Rais sio nesi kwamba aonekane kushughulikia janga la korona.”

Na pili ni kifo cha aliyekuwa Waziri wa Sheria na Katiba, Balozi Augustine Mahiga, ambapo Rais Magufuli alitangaza kumrejesha Mwigulu kwenye baraza lake la mawaziri na kumpa nafasi ya marehemu Mahiga.

Mwingine aliyeondolewa madarakani kabla ya kurudishwa ni Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Diwani Rajabu, ambaye awali “alitumbuliwa” huko Jeshi la Polisi na kuhamishiwa mkoani Kagera kuwa Katibu Tawala, kabla Rais Magufuli hajamteua kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU na baadaye kupewa ukuu wa Idara ya Usalama wa Taifa. Kwa kufanya hivyo, Rais Magufuli amemfanya Diwani kuwa “mateka wake wa kisiasa” kwani mtendaji huyo anaona uteuzi wake ni kama fadhila binafsi za Rais Magufuli kuliko uwezo wake (Diwani) kikazi.

Mhanga mwingine (na baadaye mnufaika) wa kasumba hiyo ya Rais Magufuli ni aliyekuwa kigogo wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Charles Kichere, ambaye baada ya “kutumbuliwa” na kupelekwa Njombe kama Katibu Tawala, baadaye alikumbukwa na Rais Magufuli kuwa CAG mpya, kuchukua nafasi ya Profesa Musa Assad aliyeondolewa na Rais Magufuli kinyume na taratibu kwa vile tu alizingatia vema wajibu wake wa ukaguzi na udhibiti wa mahesabu ya mapato na matumizi ya serikali.

Kwenye matumizi, Mobutu alipenda maisha ya kifahari yasiyoendana na uchumi duni wa nchi yake. Rais Magufuli nae ametokea kupenda matumizi ambayo sio tu hayaendani na uwezo wa Tanzania bali pia hayaendani na vipaumbele vya taifa hilo. Tangu aingie madarakani, Rais Magufuli amewekeza nguvu kubwa kwenye anayoita “miradi kabambe” – ujenzi wa reli ya SGR, ujenzi wa bwawa la Stiegler’s Gorge, na ununuzi wa ndege 11 hadi wakati uchambuzi huu unafanyika.

Mara kadhaa Rais Magufuli alisikika akijigamba kuwa miradi hiyo inagharamiwa kwa fedha za serikali ya Tanzania lakini baadaye ikafahamika kuwa fedha hizo ni za mikopo yenye riba kubwa.

Hata hivyo, tofauti muhimu kati ya Mobutu na Rais Magufuli ni jinsi dikteta huyo alivyoingia madarakani. Wakati Mobutu aliingia kwa mapinduzi, Rais Magufuli alishinda uchaguzi ambao hata hivyo unadaiwa kuwa ulivihujumu vyama vya upinzani.

Lakini wote wawili walitumia udhaifu uliokuwepo kabla yao kuingia madarakani. Kwa Mobutu, mtifuano wa kisiasa kati ya

Yayumkinika kuamini kuwa moja ya sababu za Rais Magufuli kujibidiisha kuidharau korona ni uwezekano wa janga hilo kuonyesha jinsi gani miaka mitano ya utawala wake ilivyokuwa na vipaumbele fyongo, kwa mfano kununua “bombadia” lukuki huku nchi nzima ikiwa na “ventilator” chache tu.

Lakini pia chuki ya Rais Magufuli kwa janga la korona inatokana na ukweli kwake ndoto yake kuona “miradi mikubwa” ikiibadili Tanzania inaelekea kuyeyuka kwa sababu kwa upande mmoja serikali yake haina uwezo wa kumudu gharama zilizopo za miradi hiyo ilhali janga la korona nalo limeathiri “mnyororo wa usambazaji” (supply chain) kitu kinachotishia kuigeuza miradi hiyo kuwa “tembo mweupe” (white elephant).

Licha ya tofauti hiyo hapo juu kuhusu kati ya Rais Magufuli na dikteta Mobutu walivyoingia madarakani, kupanda kwa wawili hao kulitokana na migogoro katika uongozi wa juu. Kwa Mobutu, kupanda kwake kulichangiwa na mgogoro kati ya Rais Joseph Kasavubu na Waziri Mkuu Patrice Lumumba.

Kwa upande wa Rais Magufuli, kufanikiwa kwake kuwa mgombea urais kwa tiketi ya CCM kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kulichangiwa na mgogoro mkubwa kuliko yote katika historia ya chama hicho tawala, kati ya aliyekuwa Kikwete na swahiba wake wa zamani Lowassa. Katika kuhofia kwamba Lowassa “angeweza kuingia Ikulu kwa mlango wa nyuma,” Kikwete alimtosa swahiba wake Bernard Membe na akamwekea ngumu January Makamba ambao pamoja na Amina Salum Ali, Asha Rose Migiro na Magufuli ndio waliopitishwa kwenye “tano bora.”

3. Kupima Dhanio (Hypothesis Testing): Hapa kuna mbinu moja tu, nayo ni Tathmini ya Madhanio Yanayoshindana (Analysis of Competing Hypotheses)

Kwa kifupi kabisa, dhanio ni kwamba “KORONA ITAMUONDOA MAGUFULI MADARAKANI.” Madhanio yanayoshindana ni mawili. Dhanio la kwanza ni hilo kwamba korona itamng’oa Rais Magufuli kutoka madarakani. Dhanio la pili ni kwamba Rais Magufuli atasalimika.

Kinachofuata ni kupima uzito na udhaifu wa kila dhanio kisha kubakiwa na dhanio lenye nguvu zaidi.

Uzito wa dhana kuwa janga la korona litagharimu uhai wa kisiasa wa Rais Magufuli unachangiwa na sababu moja kuu: urais wake umesimama kwenye msingi wa uchumi. Hata hivyo, uchumi wa nchi masikini kama Tanzania unategemea hali ya uchumi wa dunia pia. Kwa vile korona sio tu inatarajiwa kukongoroa uchumi wa dunia bali tayari athari za janga hilo kwenye uchumi limeshaonekana kwa mataifa kadhaa makubwa.

Sasa, kama ambavyo kumalizika kwa “Vita Baridi” kulivyochangia anguko la dikteta Mobutu, mtikisiko wa uchumi kutokana na janga la korona nao utaondoka na Rais Magufuli.

Udhaifu wa dhanio hili ni kwamba katika miaka mitano ya urais wake, Rais Magufuli amekuwa “survivor.” Na “survival” yake imechangiwa na jitihada zake za mapema kabisa kuhodhi madaraka ya chama na serikali na kuchomoka watu wake kila mahala. Kwa taarifa zilizopo, Rais Magufuli kwa sasa ndiye anayeendesha Idara ya Usalama wa Taifa huku Mkurugenzi Mkuu wa Idara hiyo, Diwani, akiwa kama kiongozi “ceremonial.”

Kwa kulinganisha uzito na udhaifu wa dhanio, uzito unashinda kwa sababu japo Rais Magufuli ni “survival” na amehodhi madaraka yote huko CCM na serikalini, korona ipo nje ya

mazingira ya ndani ya Tanzania. Nchi hiyo masikini inayotegemewa misaada inaweza tu kufanya baadhi ya maamuzi lakini kwa kiasi kikubwa bado ni tegemezi.

Na kama kupigilia msumari, ugomvi usio wa lazima ambao Rais Magufuli amejijengea dhidi ya nchi na taasisi wahisani pamoja na wadau wengine wa maendeleo ya Tanzania, utapelekea kukwamisha mikakati ya kujiinua kiuchumi endapo janga la korona litapoita salama.

Uzito na udhaifu wa dhana kuwa Rais Magufuli atasalimika upo kwenye kinyume cha uzito na udhaifu wa dhana kuwa janga la korona litamng'oa Rais Magufuli. Kwamba uzito ni dhana hiyo ni kwenye hoja kuwa rais Magufuli ni "survival" na amehodhi madaraka kwenye chama na serikalini, ilhali udhaifu wa dhana hiyo ni ukweli kwamba sababu zinazoweza kumng'oa Rais Magufuli zipo nje ya uwezo wake na nje ya mazingira ya Tanzania.

4. Kutengeneza Mazingira (ya kufikirika) Na Kuyafanyia Tathmini (Generating and Evaluating Scenarios):

Kwenye kutengeneza mazingira (ya kufikirika) ninatumia mbinu mbili. Ya kwanza ni Mchakato wa Roboduara (Quadrant Crunching)

Tafsiri ya mchoro huo ni hii: Kuna matokeo ya aina kuu nne hivi. Ya kwanza ni kwamba hatimaye korona inaondoka. Haijalishi ni lini lakini inaondoka kwa maana ya kuweza kudhibitiwa.

Matokeo ya pili ni korona haiondoki, inabaki nasi kwa muda mrefu kama sio milele.

Matokeo ya tatu na ya nne yanahusu uchumi. Matokeo ya tatu ni uchumi unastahimilika ilhali matokeo ya nne ni uchumi usiostahimilika.

Endapo korona itaondoka na uchumi utakuwa stahimilivu itakuwa habari njema kwa Rais Magufuli. Endapo korona haitoondoka lakini uchumi utakuwa stahimilivu (japo kidogo) ni vizuri kiasi kwa Rais Magufuli. Na endapo korona haitoondoka na uchumi hautokuwa stahimilivu, itakuwa habari mbaya kwa rais Magufuli, ilhali endapo korona itaondoka lakini uchumi utakuwa sio stahimilivu itakuwa habari mbaya japo nafuu kwa Rais Magufuli.

Mbinu ya pili ni Kujivika Uadui/Upinzani (Red Teaming). Hapa kinachofanyika ni mie kama jasusi kujivika "u-Magufuli." Kwamba, "ningekuwa Rais Magufuli ningefanyaje" katika mazingira/matokeo mbalimbali.

Lakini katika kujivika uhusika huku, ni muhimu kuzingatia "Rais Magufuli ni mtu wa aina gani." Kwa uelewa wangu, huyu ni kiongozi mbishi, asiyependa kushauriwa, anayedhani mitazamo yake tu ndiyo sahihi. Kuharibu zaidi, amezungukwa na watu wa aina mbili, kwa upande mmoja ni watendaji wazuri lakini wanaoogopa kumshauri tofauti na matakwa yake kwa kuhofia kupoteza ajira, na kwa upande mwingine ni "jamaa zake wa Kanda ya Ziwa" ambao japo walipaswa kuwa na shaka endapo urais wa jamaa yao utakuwa mashakani, wao wapo bize "kufakamia keki ya taifa."

Kwahiyo, hata "nikijivika u-Magufuli," bado haitokuwa rahisi kumbadili mtu ambaye kwa upande mmoja anajiona ni "jiwe kweli kweli," na kwa upande mwingine ana ndoto za kuwa kiongozi wa malaika pindi akiondoka duniani.

Kabla ya kuhitimisha uchambuzi huu ambao ni endelevu – kwa maana kwamba utakuwa updated mara kwa mara kulingana na maendeleo mbalimbali huko Tanzania na duniani kwa ujumla, kuna kitu kimoja ambacho japo hakihusiani moja kwa moja na yaliyochambuliwa hapo juu, kina nafasi ya kipekee katika mustakabali wa urais wa Rais Magufuli. Kitu hicho ni afya yake.

Japo hili ni suala gumu kuliongelea kutokana na unyeti wake, afya ya kiongozi huyo ni "mgogoro," na yayumkinika kuhisi kuwa inachangia katika maamuzi yake mabovu. Kwamba yawezekana

hachelei matokeo ya maamuzi yake mabovu kuhusu kushughulikia janga la korona “kwa vile matokeo hayo hayatamwathiri yeye binafsi.”

Kadhalika, janga la korona linaweza kuchangia kuzorotesha zaidi afya yake kutokana na ukweli kwamba tangu aingie madarakani hajawahi kukumbana na changamoto kubwa kama hii ya sasa, huku akifahamu fika kuwa “lundo la maadui alilotengeneza” linasubiri kwa hamu “afanye kosa moja tu la kubomoa urais wake.”

Naomba ieleweke kuwa simtabirii mabaya. Huu sio uchambuzi binafsi bali ni wa kitaalamu na kitaaluma. Masuala binafsi yanakuwa magumu kwenye mazingira kama haya lakini kwa bahati mbaya, suala la afya ya Rais Magufuli lina uzito mkubwa zaidi ya yote niliyochambua hapo juu.

Na katika hili la afya ya Rais Magufuli, ni vema kurejea tena ilivyokuwa kwenye utawala wa dikteta Mobutu ambaye licha ya kuanguka kwa utawala wake kuchangiwa na mabadiliko ya siasa za kimataifa kwa maana ya kuisha kwa “Vita Baridi,” afya yake iliyokuwa na mgogoro ilikuwa na mchango mkubwa zaidi.

Hitimisho:

Ni muhimu kutanabaisha kuwa intelijensia sio sayansi timilifu (intelligence is not an exact science). Wanasema “wiki moja tu ni sawa na uhai wa mwanadamu kwenye siasa.” Kwahiyo licha ya jitihada zangu kuangalia mazingira mbalimbali, yawezekana kabisa mambo kwenda kinyume na nilichotanabaisha hapa.

Sitarajii uchambuzi huu kupokelewa vizuri, kwa sababu zilizo wazi. Lakini si lengo la uchambuzi huu kumkera au kumfurahisha mtu yeyote yule. Lengo kuu la chapisho hili ni mchango katika uelewa (contribution to body of knowledge) katika taaluma ya intelijensia. Huenda vizazi vijavyo vya wana-intelijensia watapata kitu muhimu kutoka katika chapisho hili ambacho kitawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao.

Na endapo kuna utata kuhusu dhanio langu kwa mustakabali wa urais wa Rais Magufuli, naomba nirejee kwa kusema kuwa ninahitimisha kwamba JANGA LA KORONA LITAMNG’OA MADARAKANI.